



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BENKI KUU YA TANZANIA



MPC NA. 240

8 JANUARI 2026

Taarifa ya Kamati ya Sera ya Fedha

1. Riba ya Benki Kuu (CBR)

Katika kikao cha Kamati ya Sera ya Fedha (MPC) kilichofanyika tarehe 7 Januari 2026, kiliamua Riba ya Benki Kuu (CBR) ibaki kuwa asilimia 5.75 kwa robo ya kwanza ya mwaka 2026. Uamuzi huu umefikiwa kwa kuzingatia matarajio ya mfumuko wa bei kuendelea kuwa ndani ya lengo la asilimia 3 hadi 5. Uamuzi huo wa kubakiza CBR kama ilivyokuwa katika robo ya 4 ya mwaka 2025 utasaidia kuendelea kuchagiza ukuaji wa shughuli za kiuchumi nchini na kuwezesha ukuaji wa uchumi kuwa wa kuridhisha. Kwa kuzingatia uamuzi huu, Benki Kuu itatekeleza sera ya fedha kwa kuhakikisha riba ya mikopo ya siku 7 baina ya benki (*7-day interbank rate*) inabaki ndani ya wigo wa asilimia 3.75 hadi 7.75.

2. Tathmini ya uchumi wa dunia

2.1 Kamati ilibaini kuwa, uchumi wa dunia kwa mwaka 2025 uliendelea kuimarika kwa kasi ya kuridhisha licha ya athari zinazotokana na ongezeko la ushuru wa bidhaa za forodha, migogoro ya kisiasa, pamoja na kutokutabirika kwa matarajio ya hali ya uchumi duniani. Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) linakadiriwa ukuaji wa uchumi wa dunia kufikia asilimia 3.2 mwaka 2025, ikilinganishwa na asilimia 3.3 mwaka 2024, na unatarajiwa kuendelea kukua kwa kasi hiyo mwaka 2026. Mfumuko wa bei umeendelea kupungua na kufikia karibu au chini ya malengo ya benki kuu katika nchi nyingi, kutokana na kupungua kwa bei za nishati na utekelezaji wa sera za fedha katika nchi husika zilizopunguza viwango vya ukwasi katika vipindi vilivyopita. Kwa kuzingatia mwenendo huu, Kamati ya Sera ya Fedha inatarajia kuwa mwenendo wa uchumi wa dunia utaendelea kusaidia mfumuko wa bei nchini kubaki ndani ya lengo la mwaka 2026.

2.2 Katika robo ya nne ya mwaka 2025, bei ya mafuta ghafi ilipungua na kufikia kati ya dola 62–65 kwa pipa, na inatarajiwa kubaki katika viwango hivyo kwa robo ya kwanza ya mwaka 2026 kutokana na ongezeko la uzalishaji, sambamba na kupungua kwa mahitaji duniani. Hali hii inatarajiwa kuendelea kupunguza mfumuko wa bei na mahitaji ya fedha

za kigeni hapa nchini, na hivyo kuimarisha utulivu wa thamani ya shilingi, ikizingatiwa kwamba bidhaa za petroli huchangia takriban asilimia 17 ya gharama ya bidhaa zote zinazoagizwa kutoka nje ya nchi. Vile vile, bei ya dhahabu iliongezeka na kufikia kiwango cha juu cha dola za Marekani 4,421.65 kwa wakia, na inatarajiwa kuendelea kuongezeka katika mwaka 2026. Mwenendo wa bei ya dhahabu unatarajiwa kuongeza mapato ya fedha za kigeni na kuendelea kuimarisha thamani ya shilingi hapa nchini.

3. Tathmini ya uchumi wa ndani

3.1 Kamati ya Sera ya Fedha ilibaini kuwa uchumi wa Tanzania Bara uliendelea kukua kwa kasi ya kuridhisha ya takriban asilimia 5.9 mwaka 2025, ikilinganishwa na makadirio ya ukuaji wa asilimia 6. Ukuaji huu ulichangiwa zaidi na shughuli za kilimo, madini na ujenzi. Kwa upande wa Zanzibar, ukuaji wa uchumi wa mwaka 2026 unakadiriwa kufikia asilimia 6.8, ukichangiwa zaidi na shughuli za ujenzi, utalii na uzalishaji viwandani. Mikopo kwa sekta binafsi iliongezeka kwa wastani wa asilimia 20.3 kwa Tanzania Bara na Zanzibar. Katika robo ya kwanza ya mwaka 2026, uchumi wa Tanzania Bara unatarajiwa kukua kwa asilimia 6, na uchumi wa Zanzibar unatarajiwa kukua kwa asilimia 7.2.

3.2 Mfumuko wa bei umeendelea kuwa tulivu, ndani ya lengo la asilimia 3 hadi 5 kama ilivyokuwa imepangwa. Katika robo ya nne ya mwaka 2025, mfumuko wa bei kwa Tanzania Bara ulikuwa wa wastani wa asilimia 3.5, na kwa upande wa Zanzibar ulikuwa asilimia 3.4. Mwenendo huu mzuri ulitokana na utekelezaji madhubuti wa sera ya fedha, na mazingira mazuri ya kiuchumi duniani ambayo yalipunguza ongezeko la mfumuko wa bei kutoka nje ya nchi. Kamati inatarajia kuwa mfumuko wa bei utaendelea kubaki ndani ya lengo la asilimia 3 hadi 5 kwa robo hii.

3.3 Sekta ya benki imeendelea kuwa imara, ikiwa na ukwasi wa kutosha kuwezesha utoaji wa mikopo, pamoja na mtaji wa kutosha kuhimili misukosuko ya kiuchumi. Aidha, vihatarishi katika utoaji wa mikopo vimeendelea kupungua ambapo uwiano wa mikopo chechefu (*NPLs*) ulipungua na kufikia asilimia 3.1, chini ya ukomo unaovumilika wa asilimia 5. Mifumo ya malipo imeendelea kuwa thabiti, ikifanya kazi kwa ufanisi katika maeneo ya mijini na vijijini.

3.4 Sekta ya nje imeendelea kuimarika, ambapo nakisi ya urari wa malipo ya kawaida inakadiriwa kupungua hadi asilimia 2.2 ya Pato la Taifa (GDP) kwa mwaka 2025, ikiwa ni

kiwango cha chini zaidi katika kipindi cha miaka mitano iliyopita. Mwenendo huu mzuri ulichangiwa na kuongezeka kwa mauzo ya madini hususan dhahabu, mazao ya kilimo, kuimarika kwa shughuli za utalii na usafirishaji, pamoja na kushuka kwa bei za mafuta ghafi duniani. Kwa upande wa Zanzibar, sekta ya nje imeendelea kuwa na ziada katika urari wa malipo ya kawaida, ikichangiwa zaidi na mapato yatokanayo na shughuli za utalii.

3.5 Ukwasi wa fedha za kigeni ulikuwa wa kutosha katika robo ya nne ya 2025, kutokana na ongezeko la mapato yatokanayo na mauzo ya korosho, dhahabu na shughuli za utalii. Thamani ya shilingi iliendelea kuwa tulivu dhidi ya sarafu nyingine, huku ikiongezeka thamani kwa takriban asilimia 0.8, mwishoni wa robo ya nne ya 2025. Akiba ya fedha za kigeni ilifikia zaidi ya dola bilioni 6.3, kiasi kinachoweza kufanya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa takribani miezi 4.9, ikiwa ni juu ya lengo la angalau miezi 4. Akiba hii inatarajiwa kuendelea kuwa ya kutosha katika robo ya kwanza ya mwaka 2026, sambamba na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi na kupungua kwa bei za mafuta.

3.6 Utekelezaji wa sera ya bajeti umeendelea kuwa wa kuridhisha kwa Tanzania Bara na Zanzibar, huku makusanyo ya kodi yakiendelea kuongezeka. Deni la Serikali liliendelea kuwa himilivu, ndani ya viwango vinavyokubalika kimataifa. Tathmini ya uhimilivu wa deni kwa mwaka 2024/25 inaonesha kuwa uwiano wa deni la umma kwa Pato la Taifa (kwa thamani ya sasa) ulipungua hadi asilimia 40.6, kutoka asilimia 41.1 mwaka 2023/24, ikiwa chini ya ukomo unaokubalika kimataifa wa asilimia 55.

4. Tarehe ya kutangaza Riba ya Benki Kuu (CBR) kwa Robo Mwaka inayofuata

Kamati ya Sera ya Fedha inatarajia kukutana tena tarehe 1 Aprili 2026, na tangazo la Riba ya Benki Kuu kwa robo ya pili litafanyika siku inayofuata, tarehe 2 Aprili 2026.

Emmanuel M. Tutuba
GAVANA